


CHUO CHA SERIKALI ZA MITAA



S.L.P 1125, DODOMA Simu: 026 - 2961101, Nukushi: 026 - 2961100,
Barua pepe: info@lgti.ac.tz & Tovuti: www.lgti.ac.tz

MWALIKO WA ZABUNI YA KUPATA FUNDI SANIFU WA KUJENGA NA KUWEKA UMEME
KWA DARASA LA WANAFUNZI 400 LINALOTEGEMEWA KUJENGWA CHUO CHA SERIKALI
ZA MITAA - HOMBOLO KWA MWAKA WA FEDHA WA 2018/2019

11 Februari, 2019

1. Chuo cha Serikali za Mitaa - Hombolo kimetenga fedha kupitia vyanzo vya mapato ya ndani (Ownsource) kwa ajili ya ujenzi na uwekaji umeme katika darasa la wanafunzi mia nne (400) kwa mwaka wa fedha **2018/2019** ambapo inategemewa kuwa shughuli hizo zitafanyika kwa nguvu kazi (Force Account Procurement Method). Inakusudiwa kuwa sehemu ya fedha hizo zitatumika kugharamia malipo halali chini ya mikataba ambayo itatolewa katika Mwaliko wa Zabuni hii.
2. Hivyo, Chuo kinakaribisha maombi toka kwa mafundi mbalimbali wakiwa ni mtu binafsi au kikundi kinachotambulika na kusajiliwa kisheria kufanya kazi zilizokusudiwa katika ujenzi wa darasa lenye uwezo wa kutumiwa na wanafunzi mia nne (400) katika Chuo Cha Serikali za Mitaa - Hombolo kwa mchanganuo ufuatao;

Na.	Namba na Maelezo ya Zabuni	Uhitaji wa Zabuni	Ada ya kulipia Zabuni (Tshs)
01	PA/080/2018/2019/W/01; Kwa ajili ya Ujenzi wa Darasa la kutumiwa na wanafunzi 400.	Gharama ya ufundi wa ujenzi (Local Fundi) kwa kuzingatia Nyaraka ya Zabuni.	50,000.00
02	PA/080/2018/2019/W/02; Kwa ajili ya Uwekwaji/ufungwaji wa umeme katika Darasa la kutumiwa na wanafunzi 400.	Gharama ya ufundi wa umeme (Local Fundi) kwa kuzingatia Nyaraka ya Zabuni.	20,000.00

3. Waombaji watanunua vitabu vya zabuni na kupata maelezo ya zabuni husika katika Ofisi ya Mkuu wa Chuo kupitia Kitengo Cha Manunuzi na Ugavi kuanzia saa mbili kamili (2:00) asubuhi mpaka saa tisa kamili (9:00) jioni, Jumatatu mpaka Ijumaa isipokuwa siku za mapumziko.
4. Kitabu cha Zabuni kitauzwa kwa gharama inayozingatia aina ya Zabuni kwa mchanganuo hapo juu ambayo haitarejeshwa kwa mwombaji. Malipo hayo yafanywe kupitia Akaunti ya Chuo kwa Benki ya NMB baada ya kupewa namba ya malipo (Control Number). Baada ya kufanya malipo kwa ukamilifu utapatiwa stakabadhi ya mfumo itakayo wasilishwa Kitengo Cha Manunuzi kwa ajili ya kupata kitabu cha Zabuni.
5. Maombi yote yaambatane na barua ya kuomba Zabuni na barua ya mdhamini mwenye mali isiyo hamishika au dhamana ya Taasisi ya Kifedha.
6. Kila mwombaji anatakiwa kurejesha Kitabu cha Zabuni katika uhalisia wake (Original) na nakala (Copy) moja zilizojazwa kwa usahihi na kuwekwa kwenye bahasha isiyo na maandishi kwa kila moja na kuwekwa katika bahasha moja iliyoandikwa " Namba ya Zabuni pamoja na Jina la Zabuni". Nilazima Zabuni zote wakati wa kurejeshwa zipelekwe Ofisi ya Kitengo cha Manunuzi na Ugavi.
7. Maombi yote yafungwe vizuri kwenye bahasha na kutumwa kwenye anuani ifuatayo hapa chini,

**Katibu wa Bodi ya Zabuni,
Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo,
S.L.P 1125,
DODOMA.**

8. Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe **18 Februari, 2019** siku ya **Jumatatu** saa **8.00** kamili Mchana na baada ya hapo maombi hayo yatafunguliwa mbele ya waombaji au wawakilishi wa waombaji katika Ukumbi wa Maktaba kuu ya Chuo cha Serikali za Mitaa.
9. Zabuni zitakazo chelewa, zitakazo tumwa kielektroniki na zisizofunguliwa katika kikao cha ufunguzi wa Zabuni, hazitakubaliwa kwa ajili ya zoezi la tathmini na hatua zingine za mchakato wa Zabuni.



Dr. Mpamila Madale

MKUU WA CHUO